



**HALMASHAURI YA WILAYA YA MBINGA**

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb.Na.** MDC/S.50/7/155

**Tarehe:** 02 Machi, 2023

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga anapenda kuwatangazia watanzania wote wenye sifa kutuma maombi kwa nafasi zifuatazo:-

**MTENDAJI WA KIJIKI III - NAFASI 05**

**1. SIFA ZA MWOMBAJI:**

Kuajiriwa wenye cheti cha kidato cha nne (IV) au sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/ Cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**2. KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI III:**

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamzi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- vi. Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa Kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji.
- viii. Kusimamia, kukusanya na kihifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji.
- ix. Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji.
- x. Kupokea, Kusikiliza na Kutatua malalamiko na migogoro ya Wananchi.
- xi. Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za Kijiji na
- xii. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

**3. MSHAHARA:**

Cheo cha Mtendaji wa Kijiki III kina mshahara wa TGS B kwa mwezi.


**4. MASHARTI YA JUMLA:**



- Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa.
- Mwombaji ambaye ni mtumishi wa Umma apitishe maombi yake kwa mwajiri wake.
- Mwombaji aambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika pamoja na namba zao za simu.
- Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya Elimu na Taaluma kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.
- "Testimonials", "Provisional Results" "Statements of results" nk. Hazitakubalika.
- Waombaji waweke picha moja katika barua zao za maombi.
- Waombaji wote ambao wamesoma nje ya nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na TCU na NECTA.
- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni **tarehe 15/03/2023** saa 9:30 Alasili.
- Barua zote zitumwe kwa anwani iliyopo hapo chini:-

Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,  
Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga,  
239 Barabara ya Mbambabay,  
S. L. P 194,  
**57483, Kigonsera , RUVUMA**

**NB:** Tangazo hili pia linapatikana kwenye tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ambayo ni:- [www.mbingadc.go.tz](http://www.mbingadc.go.tz)



Juma Haji Juma  
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**MBINGA**

**Nakala:** Katibu,  
Ofisi ya Rais,  
Sekretarieti ya Ajira katika  
Utumishi wa Umma,  
Jengo la Utumishi (UDOM),  
Eneo la Dr. Asha Rose Migiro  
S.L.P. 2320,  
**DODOMA.**

“ **Mbao za Matangazo**